SHIRIKA LA KUWEZESHA MAENDELEO (ADP MBOZI)

TOKEO LA TATU: ***Lishe ya kaya (hasa watoto) imeboreshwa.***

- Kutambua kaya zenye watoto chini ya miaka mitano.
- Kutambua vyakula vya asili katika eneo la mradi.
- Kufundisha wakulima mbinu bora za utunzaji wa bustani na matunda.
- Kufundisha wakulima kilimo bora cha soya.
- Kufundisha kwa vitendo usindikaji wa soya na mbogamboga.
- Kufundisha kwa vitendo utayarishaji wa mlo uliokamilika.
- Kuwezesha siku ya chakula duniani.

Uzalishaji matunda

TOKEO LA NNE: ***Uelewa wa masuala ya jinsia na UKIMWI umehuishwa kwenye shughuli za mradi***

- Kuendesha mikutano ya kuwatambua walengwa watakaopewa mafunzo ya Waraghabishi.
- Kuendesha mafunzo kwa Waraghabishi.
- Kuwezesha Waraghabishi ili waweze kutekeleza majukumu yao.
- Kuendesha mafunzo rejea kwa Waraghabishi.
- Kuwezesha ziara za mafunzo kwa Waraghabishi.
- Kuendesha mikutano ya ufahamu kwa walengwa kuhusu jinsia na bajeti ya chakula na namna UKIMWI unavyoweza kuathiri nguvu kazi katika uzalishaji wa chakula.
- Kufundisha wakulima matumizi bora ya wanyama kazi katika uzalishaji wa chakula.
- Kuwezesha walengwa kushiriki siku ya wanawake duniani.
- Kuwezesha walengwa kushiriki siku ya UKIMWI duniani.

MBINU ZA UTEKELEZAJI:

- Kufanya kazi na walengwa kupitia vikundi.
- Kufanya kazi kupitia mitandao/ asasi za walengwa.
- Kutumia mashamba darasa.
- Kutambua wakulima wawezeshaji (**Wagani kazi na Waraghabishi**) kwa kuwapa mafunzo ili wasaidie kazi vijijini.
- Kufanya kazi na wakulima waliochaguliwa kwa utaratibu maalumu kwa njia ya mkataba shirikishi.
- Kufanya ufuatiliaji wa pamoja yaani walengwa, wataalamu wa shirika na wale wa serikali.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi Mtendaji,
Shirika la ADP Mbozi

Makao Makuu
S. L. P. 204, Mbozi, Mbeya.
Simu. +255 (025)-2580095
& +255 0754 398342 & 0759 490037
Tawi la Makongorosi – Chunya
Simu: 0767 072060
Tawi la Kanga – Songwe
Simu: 0754 578614

Tawi la Njombe
S. L. P. 40, Ilembula, Njombe.
Nukushi: +255 (025) 2580312
Barua pepe: info@adpmbozi.or.tz & adpmbozi@yahoo.com
Tovuti: www.adpmbozi.or.tz

MRADI WA UHAKIKA WA CHAKULA MOMBA NA SONGWE

Julai 2016 – Desemba 2018

Unaotekelezwa na

SHIRIKA LA KUWEZESHA MAENDELEO (ADP MBOZI)

Tupo kwa ajili ya kupambana na umaskini vijijini na mjini

SHIRIKA LA KUWEZESHA MAENDELEO (ADP MBOZI)

Baadhi ya viongozi na watumishi wa Shirika

UTANGULIZI

Shirika la ADP-Mbozi lilianza kama mradi hapo mwaka 1986 na liliandikishwa rasmi kama Mfuko wa Udhamini tarehe 29/11/1995. Hatimaye tarehe 10/10/2005 Shirika lilisajiliwa chini ya sheria ya mashirika yasiyo ya kiserikali Tanzania; sheria namba 24 ya mwaka 2002. Namba ya uandikishwaji ya Shirika ni 1639. ADP –Mbozi ni kifupi cha maneno “Actions for Development Programs – Mbozi”.
Shirika lilianza kwa kutekeleza mradi wa uhakika wa chakula katika tarafa ya Vwawa, Mbozi na limeendelea kupanua maeneo ya kutoa huduma na pia kupanua aina za huduma**.**

Katika mpango mkakati wa mwaka 2014 – 2016, Shirika linatekeleza programu zake katika vipaumbele vifuatavyo;-

1. Kilimo endelevu na matumizi ya chakula.
2. Ujasiriamali na uendelezaji masoko.
3. Utunzaji wa mazingira.
4. Uhamasishaji jamii (Jinsia, VVU na UKIMWI na Utawala Bora).
5. Maendeleo ya Shirika.

MRADI WA UHAKIKA WA CHAKULA MOMBA NA SONGWE

Mradi wa uhakika wa chakula Momba na Songwe uliandaliwa kwa kushirikiana na wananchi wa kata saba wilayani Songwe na kata nne wilayani Momba ili kukabili tatizo la njaa linalojitokeza mara kwa mara katika kata hizo. Chimbuko la mradi huu ni utekelezaji wa mafanikio wa mradi wa uhakika wa chakula Momba awamu ya tatu ambao nao ulitokana na awamu ya kwanza na ya pili ya miradi ya uhakika wa chakula Myunga na Chitete. Mradi huu unafadhiliwa kwa pamoja na mashirika ya ADA, DKA, Welthaus Graz na HORIZONT3000 ya Austria. Huu ni mradi wa miaka miwili na nusu kuanzia Julai 2016 hadi Desemba 2018.

LENGO KUU LA MRADI

Kuongeza uhakika wa chakula katika katika kata 11 za wilaya za Momba na Songwe ifikapo mwaka 2018.

MALENGO MAHUSUSI YA MRADI

1. Kuongeza uzalishaji wa mazao na mifugo ifikapo Desemba 2018.
2. Kuboresha hifadhi ya mazao na bajeti ya chakula ifikapo Desemba 2018.
3. Kuboresha matumizi ya chakula katika kaya ifikapo Desemba 2018.

MATOKEO NA SHUGHULI ZA MRADI

TOKEO LA KWANZA*: Wakulima wamefundishwa mbinu bora za uzalishaji wa mazao na mifugo na wanazitumia.*

- Kuendesha mashamba darasa ya mazao katika kila kijiji kwa ajili ya mazao na mifugo.
- Kufundisha wakulima mbinu bora za uzalishaji wa mazao na mifugo.
- Kufundisha wakulima upimaji wa mashamba na mavuno.
- Kuwezesha ziara za mafunzo ndani na nje ya eneo la mradi.
- Kuwezesha wakulima kuandaa mbegu bora za daraja la kuazimia.
- Kuendesha mikutano ya kuwatambua walengwa watakaopewa mafunzo ya Waganikazi.
- Kuandaa Wagani kazi
- Kuunganisha wakulima na wasambazaji wa pembejeo

Kilimo bora cha mahindi

TOKEO LA PILI: *Mbinu za kuhifadhi mazao na kuweka bajeti ya chakula katika kaya zimeboreshwa.*

- Kufundisha wakulima mbinu za asili na za kisasa za kuhifadhi mazao.
- Kuwezesha ziara za mafunzo katika maeneo ya jirani.
- Kuhamasisha wakulima kuhusu uwekaji wa bajeti ya chakula.
- Kufundisha wakulima ukokotoaji wa bajeti ya chakula.
- Kufundisha matumizi ya fomu ya bajeti ya chakula iliyoboreshwa.

Uwekaji wa bajeti ya chakula